



KIJARIDA KUHUSU

TARATIBU ZA RUFAA

KUTOKA MAHAKAMA KUU

KWENDA MAHAKAMA YA

RUFAA

Kwa Jamii yenyeye Haki na Usawa





**Unaweza kutoa taarifa
za ukiukwaji wa haki
kupitia**

#HakiKiganjani



0699695486



Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**



hakikiganjani.humanrights.or.tz

Usipotezee, toa taarifa sasa!



TARATIBU ZA RUFAA KUTOKA MAHAKAMA KUU KWENDA MAHAKAMA YA RUFAA

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

YALIYOMO

SHUKRANI	5
DIBAJI	5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....	7
MAONO	8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI	8
LENGO KUU	8
1. Utangulizi.....	9
2. Hatua za kufuata pindi unapotaka kukata rufaa	10
3. Ruhusa (leave) na uthibitisho wa suala la kisheria (certification on point of law).....	14
4. Kuwasilisha sababu za rufaa na kumbukumbu za rufaa.	19
5. MAJUMUISHO YA MAANDISHI	23
6. HITIMISHO.....	25

SHUKRANI

Tunatoa shukrani za dhati kwa wanasheria wetu Wakili Hamisi Mayombo na Wakili Neema Jaji pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hususani ofisi ya Arusha kwa kukiandaa kijitabu hiki.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi

kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia

kwa karibu. Umalizapo, tafadhalii umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam. Pia Kituo kina ofisi nyingine Arusha na Dodoma

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

1. Utangulizi

Taratibu za kukata rufaa kutoka mahakama kuu kwenda mahakama ya rufaa zina utofuati mkubwa ukilinganisha na zile za mahakama za chini kuja mahakama kuu. Hii inasababishwa na mambo mengi kufanyika ikiwa pamoja na kufanya maombi mbalimbali kabla ya rufaa husika kukatwa. Kutohana na hali hiyo watu wengi wamekuwa wakipata changamoto na vikwazo vingi wanapohitaji kukata rufaa kwenda mahakama ya rufaa. Halihii inawatokea zaidi watu ambao hawana uwakilishi wa mawakili kwani wengi wao wanashindwa kabisa kufika mahakama ya Rufaa au wale wanaofika rufaa zao hutupiliwa mbali kutohana na kushindwa kukidhi matakwa mbalimbali ya kisheria. Hivyo kutohana na hali hiyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeamua kutayarisha kijarida hichi ili kumrahisishia msomaji na jamii kwa ujumla kuelewa hatua zippi za kufuatwa pale mtu asiporidhishwa na maamuzi ya mahakama kuu. Taratibu za

kukata rufaa kutoka Mahakama Kuu kwenda Mahakama ya Rufaa katika mashauri ya madai zinasimamiwa na sheria tofauti tofauti ikiwemo Sheria ya Mamlaka ya Rufaa Sura namba 141 (The Appellate Jurisdiction Act Chapter 141), kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 2009 (iliyorejewa 2019), pamoja na maamuzi mbalimbali ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu ya Tanzania.

2. Hatua za kufuata pindi unapotaka kukata rufaa

Mtu yejote anayetaka kukata rufaa kwenda mahakama ya rufaa atahitajika kufuata tarataibu zifuatazo kwa mpangilio bila kuruka hata moja. Vilevile taratibu hizo zinatakiwa kufuatwa ndani ya muda uliowekwa na sheria pamoja na kanuni zake.

i. Notisi ya Kukusudia Kukata Rufaa

Mtu yeьте anayetaka kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa ya Tanzania atahitajika kuwasilisha notisi ya maandishi kwa msajili wa mahakama kuu ndani ya siku thelathini (30) toka tarehe ambayo maamuzi ya mahakama kuu yametolewa. Kila notisi ya rufaa ni lazima ieleze kama mkata rufaa amedhamiria kupinga maamuzi yote au sehemu tu ya maamuzi husika. Na kama mkata rufaa amedhamiria kupinga sehemu tu ya maamuzi husika basi atahitajika kuielezea kinaga ubaga sehemu hiyo. Notisi pia inatakiwa ioneshe anuani ya mkata rufaa pamoja na majina na anuani za watu wote ambao notisi hiyo itapelekwa.

Notisi ya Rufaa inatakiwa kusainiwa na mkata rufaa mwenyewe au mwakilishi wake ambaye anaweza kuwa wakili au mtu mwingine ambaye sheria inamruhusu.

Mkata rufaa analazimika kuipeleka notisi ya rufaa kwa watu ambao wanahuksika au wanaathirika moja kwa moja na rufaa hiyo

kabla au ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku ambapo imewasilishwa mahakamani. Kama mtu ambaye analazimika kupelekewa notisi ya rufaa na hakutoa anuani nyingine kwa ajili ya rufaa basi aliyokuwa anaitumia mahakama kuu ndiyo itatumika hata kama itakuwa ni ya wakili ambaye hajapata maelekezo ya kuwakilisha kwenye rufaa.

Mtu yoyote ambaye notisi ya rufaa ilipelekwa kwake atatakiwa ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku ambayo ameipokea atatakiwa kuwasilisha notisi inayoonesha anuani yake katika masijala ya mahakama husika pamoja na kuipeleka kwa mkata rufaa. Vilevile taratibu zinamhitaji mtu ambaye amewasilisha notisi ya anuani ndani ya siku kumi na nne (14) zingine kuzipeleka kwa watu wengine wote ambao wametajwa katika notisi ya rufaa. Kama ilivyo kwa notisi ya rufaa, notisi ya anuani itawekwa sahihi na huyo mtoa anuani au na mwakilishi wake.

Ifahamike kuwa notisi ya rufaa haitakuwa batili

au kuharibika pale itakapotokea aliyepelekewa notisi hiyo amefariki, sheria inasema nakala ya notisi ipelekwe kwa mwakilishi wa marehemu anayetambulika kisheria haraka iwezekanavyo. Siyo lazima kuambatanisha nakala ya hukumu au maamuzi wakati wa kufaili notisi ya rufaa.

ii. Maombi ya nakala za mwenendo

Sambamba na kuwasilisha notisi ya kukusudia kukata rufaa, mkata rufaa anatakiwa kupeleka maombi ya nakala za mwenendo kwa msajili wa mahakama kuu ndani ya siku thelathini (30) toka siku ambapo mahakama kuu imetoa maamuzi. Mkata rufaa anatakiwa kuunganisha sababu za rufaa pamoja na nakala za kumbukumbu ya mwenendo toka shauri lilipoanza mpaka lilipofikia kama ilivyoainishwa katika kanuni ya tisini na sita (96) ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa za mwaka 2009.

3. Ruhusa (leave) na uthibitisho wa suala la kisheria (certification on point of law)

Baada ya kuwasilisha notisi ya kukusudia kukata rufaa mkata rufaa atahitajika kufuata taratibu zingine kadri sheria husika au maamuzi mbalimbali ya Mahakama ya Rufaa na Mahakama kuu yatakavyokuwa yanaagiza. Kuna rufaa ambazo zinahitaji ruhusa (leave) au uthibitisho wa uwepo wa jambo la kisheria (certification on point of law) wa mahakama kuu ili uweze kuwasilisha rufaa katika Mahakama ya Rufani. Pia kuna rufaa ambazo mkata rufaa atawasilisha rufaa yake moja kwa moja bila ya kuhitaji ruhusa au uthibitisho pointi ya kisheria kutoka Mahakama Kuu.

i. Maombi ya Ruhusa/Idhini (leave).

Mtu yoyote ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mahakama Kuu ambayo yameanzia Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

baada ya kuwasilisha notisi ya rufaa, atahitajika kufanya maombi ya ruhusa au idhini (leave) Mahakama Kuu. Maombi ya kuomba ruhusa/ idhini (leave) kwenda mahakama ya rufani yanatakiwa yafanyike ndani ya siku kumi na nne (14) kutoka siku ambayo mahakama kuu imetoa maamuzi husika. Kama itatokea mtu amechelewa kufanya maombi hayo ndani ya muda uliowekwa, basi atahitajika kuomba kupeleka maombi ya ruhusa/idhini nje ya muda.

Endapo maombi ya ruhusa/idhini (leave) au maombi ya kufanya maombi ya ruhusa/idhini (leave) nje ya muda yatakataliwa na mahakama kuu basi mkata rufaa anaruhusiwa kuomba tena maombi hayo katika mahakama ya rufani. Hapa ifahamike kwamba endapo mahakama kuu itamnyima mkata rufaa ruhusa (leave) na ye ye hakuridhika basi mkata rufaa hahitajiki kukata rufaa kwenda mahakama ya rufaa bali sheria inataka maombi hayo yawasilishwe mara ya pili (second bite) katika mahakama ya

rufani ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku ya maamuzi.

ii. Maombi ya uthibitisho wa uwepo wa suala la kisheria (certification on point of law).

Ukitoa uhitaji wa ruhusa/ihini (leave) kwenye rufaa zinazoanzia Mahakamaya Wilaya, Hakimu Mkazi na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, vilevile kuna rufaa zinazohitaji uthibitisho wa uwepo wa suala la kisheria (certification on point of law) na Mahakama Kuu kabla ya rufaa kuwasilishwa Mahakama ya Rufaa. Hizi ni zile rufaa zilizoanzia Mahakama ya Mwanzo au Baraza la Kata hadi kufika Mahakama Kuu. Endapo mtu hatokuwa ameridhishwa na maamuzi ya Mahakama Kuu basi baada ya kuwasilisha notisi ya kukusudia kukata rufaa atahitajika kufanya maombi ya uthibitisho wa uwepo wa suala la kisheria mahakama kuu ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku ambayo maamuzi yamefanywa na Mahakama Kuu.

Mkata rufaa anatakiwa afahamu kwamba rufaa zinazoanzia Mahakama ya Mwanzo zitaruhusiwa kwenda mahakama ya rufaa pale Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani itakapojiridhisha kwamba suala la kisheria moja au zaidi lilikosewa mahakama za chini au Mahakama Kuu. Hivyo kwenye maombi yake atahitajika kuionesha hiyo pointi ya kisheria. Endapo Mahakama Kuu itayatupilia mbali maombi hayo na kama mleta maombi atakuwa hajaridhika basi sheria inampa nafasi ya kuleta maombi hayo kwa mara ya pili (second bite) katika Mahakama ya Rufani. Ikumbukwe mleta maombi haruhusiwi kukata rufaa endapo maombi yake yatatupiliwa mbali na Mahakama Kuu.

iii. Rufaa isiyohitaji ruhusa/ihini (leave) wala uthibitisho wa uwepo wa suala la kisheria (certification on point of law)

Mashauri yote ambayo yanaanza Mahakama Kuu hayahitaji ruhusa wala uthibitisho wa uwepo wa suala la kisheria pale mtu anapotaka

kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani. Baada ya kuwasilisha notisi ya kukusudia kukata rufaa basi mkata rufaa anaruhusiwa moja kwa moja kupeleka sababu zake za rufaa Mahakama ya Rufani.

iv. Rufaa katika mashauri ya Ajira na Kazi

Vilevile lazima ifahamike kwamba mashauri yote yanayohusu ajira ambayo mara nyingi huanzia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na baadaye Mahakama Kuu Kitengo cha Kazi hayaitaji ruhusa (leave) au uthibitisho wa uwepo wa jambo la kisheria pale mtu anapohitaji kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani.

Na vilevile inapaswa ifahamike kwamba baada ya nakala za mwenendo wa shauri kuombwa kwa Msajili, basi msajili atatakiwa ndani ya siku tisini (90) toka siku ambapo nakala husika zimeombwa awe amemtaarifu mkata rufaa kwenda kuchukua nakala hizo. Endapo itatokea siku tisini zimekwisha bila ya msajili kumtaarifu mrufani kuchukua nakala hizo basi mkata rufaa atalazimika kwenda kuzifuatlia nakala hizo.

4. Kuwasilisha sababu za rufaa na kumbukumbu za rufaa.

Baada ya kufanya taratibu zote zilizotajwa hapo juu mkata rufaa anatakiwa awasilishe sababu zake za rufaa ndani ya siku sitini (60) toka tarehe ambayo notisi ya rufaa imewasilishwa mahakamani. Pamoja na sababu za rufaa, mkata rufaa atahitajika kuwasilisha kumbukumbu za mwenendo wa rufaa (records of appeal) na dhamana ya gharama za rufaa (security for the costs of appeal). Kama mkata rufaa atakuwa amechelewa kuwasilisha rufaa yake katika muda uliowekwa kwasababu ya kuchelewa kupata nakala za kumbukumbu ya mwenendo wa shauri, siku za rufaa zitatakiwa kuhesabiwa kuanzia tarehe ya kupata nakala za kumbukumbu za mwenendo lakini zitatakiwa kuthibitishwa na Msajili wa Mahakama Kuu. Hivyo mkata rufaa ataomba kuongezewa muda kwa msajili ili kupata cheti cha kuchelewa (Certificate of Delay).

Mkata rufaa atatakiwa kabla au ndani ya siku saba (7) baada ya kuwasilisha sababu za rufaa na kumbukumbu za mwenendo wa rufaa kupeleka nakala hizo kwa mjibu rufaa.

Lakini vilevile mkata rufaa atatakiwa kupeleka nakala ya sababu za rufaa na kumbukumbu za mwenendo kwa wahusika wengine ambao walikuwepo kwenye shauri lilipoanza mahakama za chini. Hii inaweza kufanyika kwa amri ya mahakama pale maombi yanapopelekwa au kwa mahakama yenyewe kwa utashi wake pale itakapoona inafaa.

i. Kumbukumbu za rufaa kwa mashauri yalioanzia Mahakama Kuu.

Kumbukumbu za rufaa kwa mashauri yalioanzia Mahakama Kuu zinahitaji kuwa na nakala zifuatazo kabla hazijawasilishwa Mahakama ya Rufani

- Orodha itakayoonyesha idadi na majina ya nakala zote ambazo zimeambatanishwa pamoja na namba ya ukurasa ambapo nakala husika inapatikana

- Nakalaitakayooneshaanuaniyamkatarufaa na anuani ya mjibu rufaa kama alivyoitoa ye ye mwenyewe wakati alipopelekewa notisi ya rufaa. Kama itatokea mjibu rufaa hakuwasilisha anuani wakati alipopewa nakala ya notisi ya rufaa basi itaoneshwa anuani yake ya mwisho iliyotumika kumpelekeka nakala za kimahakama na uthibitisho wa kupelekewa notisi ya rufaa.
- Hati za madai, hati kinzani na nakalazingine zozote zinazoendana na hizo (Pleadings)
- Kumbukumbu za mwenendo wa shauri
- Muhtasari wa maelezo mafupi yoyoyte yaliyochukuliwa wakati wa shauri.
- Viapo vilisomwa na nakala zote zilizotumika kama Ushahidi wakati wa kusilikiza shauri na kama nakala hizo hazipo kwa lugha ya kiingereza pamoja na nakala zilizotafsiri.
- Maamuzi (Ruling and Judgment)
- Amri (decree and order)
- Amri ya ruhusa ya kukata rufaa kama kulikuwa na takwa hilo kisheria
- Notisi ya rufaa

- Na nakala nyingine yoyote ambayo itaonekana ina ulazima kuwepo katika kufanya maamuzi ya rufaa ikiwemo nakala za mwenendo wa maombi madogo katika shauri husika kama itaonekana inahusika moja kwa moja.

ii. Kumbukumbu za rufaa kwa shauri lililoanzia mahakama za chini

Kwa rufaa ambayo imeanzia mahakama za chini yaani Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakamaya Wilaya au Mahakama ya Mwanzo au kwenye mabaraza. Kwa aina hii ya rufaa nakala ambazo zinatakiwa kuambatanishwa ni zile zinazofanana na rufaa ambayo imeanzia mahakama kuu kama ilivyoainishwa hapo juu. Lakini nakala zifuatazo zilizotumika kwenye usikilizwaji wa rufaa katika mahakama ya rufaa ya kwanza lazima ziambatanishwe ambazo ni

- Amri ya kutoa ruhusa ya kukata rufaa kama kuna takwa hilo la kisheria
- Sababu za rufaa
- Kumbukumbu za mwenendo

- Maamuzi (Ruling and Judgment)
- Amri (decree and order)
- Notisi ya rufaa

Hapa lazima ikumbukwe kuw kama kesi imepelekwa kama rufaa ya tatu yaani imeanzia Mahakama ya Mwanzo au Baraza la Kata basi nakala zilizotumika kwenye rufaa ya pili zitatakiwa kuambatanishwa. Na vilevile nakala ya uthibitisho wa suala la kisheria kama ilivyothibitishwa na Mahakama Kuu nayo itatakiwa kuambatanishwa.

5. MAJUMUISHO YA MAANDISHI

Ndani ya siku sitini (60) baada ya kuwasilisha sababu na kumbukumbu za rufaa mkata rufaa au mjibu rufaa atatakiwa kufaili majumuisho ya maandishi ya kufafanua au kupinga rufaa hiyo. Kwenye majumuisho hayo ya maandishi mkata rufaa au mjibu rufaa atatakiwa kuonyesha vitu vifuatavyo:

i. Maelezo ya shauri lilipoanza mpaka kufikia

kwenye rufaa.

- ii. Maelezo yanayohusu hoja au sababu zilizoibuliwa kwenye rufaa yake. Kama mkata rufaa atakuwa ameamua kuondoa moja au zaidi katika sababu zake za rufaa basi atahitajika kueleza katika majumuisho hayo. Hapo pia, kama mkata rufaa atakuwa na nia ya kuomba kuongeza sababu nyingine ambayo haikuwemo kwenye sababu za rufaa zilizowasilishwa mahakamani hapo awali basi atahitajika kuonyesha kwenye majumuisho hayo.
- iii. Maelezo ya hoja au maswali ambayo mkata rufaa angependa mahakama iyazingatie.
- iv. Sheria au kanuni za sheria ambazo zina mahusiano na sababu za rufaa zilizowasilishwa mahakamani.

6. HITIMISHO

Kwa kuhitimisha, taratibu za kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani zinahitaji uangalifu mkubwa ambapo kuna mahitaji ya kisheria ambayo lazima yafuatwe. Lakini uzoefu unaonyesha kwamba imekuwa ni vigumu kwa mtu asiyekuwa na ujuzi wa kisheria kuweza kuzifuata taratibu hizo bila kukosea. Kwani ukitoa masharti yaliyoainishwa hapo juu kuna vitu vingine vingi ambavyo mtu atahitaji kuvifanya. Hivyo inapofika kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani mtu anashauriwa kutafuta mwanasheria au kama atakuwa hana uwezo wa kifedha basi atafute usaidizi kwenye taasisi zinazotoa msaada wa kisheria kama Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.



Norwegian Embassy



Ministry for Foreign
Affairs of Finland

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)

Jengo la Jaji Lugakingira,

S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037

Barua Pepe: lhrc@humanrights.or.tz

Tovuti: www.humanrights.or.tz

KITUO CHA MSAADA WA SHERIA

Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania

Simu/Nukushi: +255 22 2761205/6

Barua Pepe: legalaid@humanrights.or.tz

OFISI YA ARUSHA

Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,

S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187

Barua Pepe: lhrcarusha@humanrights.or.tz

OFISI YA DODOMA

Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania

Simu/Nukushi: +255 262350050

Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz

